**HOTUBA YA MHESHIMIWA KASSIM M. MAJALIWA (MB.), WAZIRI MKUU WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA WAKATI WA KUAHIRISHA MKUTANO WA 17 WA BUNGE LA 12 TAREHE 8 NOVEMBA, 2024 DODOMA**

## UTANGULIZI

### Shukrani

1. ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** awali ya yote ninamshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa rehema zake zilizotufikisha katika siku ya leo mahsusi kwa ajili ya kuhitimisha shughuli za Mkutano wa 17 wa Bunge la 12 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

2. ***Mheshimiwa Naibu Spika***, nitumie fursa hii, kutambua kazi kubwa inayofanywa na Mheshimiwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuliongoza Bunge kwa weledi mkubwa. Sina shaka Waheshimiwa Wabunge wenzangu watakubaliana nami kwamba viwango vya umahiri vya Mheshimiwa Spika vimeendelea kuongezeka, na kwa kila Mkutano tumeendelea kushuhudia hekima kubwa ambayo imefanya vikao vyote kumalizika kwa mujibu wa ratiba iliyopangwa.

3. ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** vilevile, ninatambua mchango wako wewe binafsi pamoja na Waheshimiwa Wenyeviti wa Bunge ambao ni Mheshimiwa Najma Murtaza Giga (Mb.), Mheshimiwa Joseph Kizito Mhagama (Mb.) na Mheshimiwa Deodatus Phillip Mwanyika (Mb.) katika kuliongoza Bunge letu tukufu.

4. ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** leo tunapohitimisha Mkutano huu wa 17 wa Bunge la 12 tunafahamu kuwa wewe pamoja na Wasaidizi wako mmekuwa chachu ya mafanikio ya Mkutano huu. Kwa niaba ya Waheshimiwa Wabunge wenzangu tunawashukuru sana na tunamwomba Mwenyezi Mungu azidi kuwapa nguvu na hekima ya kulitumikia Bunge hili.

5. ***Mheshimiwa Naibu Spika***, nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sitawashukuru Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa kazi kubwa waliyoifanya katika mkutano huu. Serikali kupitia Waheshimiwa Mawaziri tumepokea maoni, ushauri na hoja zilizowasilishwa na Waheshimiwa Wabunge. Nikiri kwamba wakati wote michango ya Waheshimiwa Wabunge katika mijadala mbalimbali imekuwa na tija sana kwa Serikali.

6. ***Mheshimiwa Naibu Spika***, nitumie nafasi hii kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa, Serikali imepokea michango yote na itaifanyia kazi kwa mustakabali wa maendeleo ya wananchi wote wa Tanzania.

### Salamu za Pole

7. ***Mheshimiwa Naibu Spika***, tangu kuahirishwa kwa Mkutano wa 16 wa Bunge la 12 yapo majanga yaliyotokea hapa nchini na kusababisha athari mbalimbali kwa Watanzania wenzetu. Nitumie nafasi hii kutoa pole kwa Watanzania wote waliopatwa na majanga hayo au waliopoteza wapendwa wao na uharibifu wa

mali. Kwa wale waliojeruhiwa ninamwomba Mwenyezi Mungu awape uponyaji wa haraka. **Amin!**

**8.** ***Mheshimiwa Naibu Spika***, tarehe 29 Oktoba 2024 tulipokea kwa masikitiko taarifa ya kifo cha Jenerali David Bugozi Musuguri aliyewahi kuwa Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi, ninatoa pole kwa familia, ndugu, jamaa, marafiki na Watanzania wote kwa msiba huo. Jenerali Musuguri atakumbukwa kwa ujasiri na utumishi uliotukuka katika Jeshi la Wananchi.

**9.** ***Mheshimiwa Naibu Spika***, vilevile, tarehe 2 Novemba, 2024 tuliondokewa na Jaji Mstaafu wa Mahakama ya Rufani, Mheshimiwa Kipenka Msemembo Musa aliyewahi kutumikia kwa nyakati tofauti mihimili yote ya dola. Kama mtakumbuka Mheshimwa Kipenka aliwahi kulitumikia Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika nafasi ya Katibu wa Bunge kuanzia mwaka 2000 hadi 2004. Ninatoa pole kwa familia, ndugu, jamaa, marafiki na Watanzania wote. Mheshimiwa Kipenka atakumbukwa kwa mchango wake mkubwa kwa nafasi zote alizozitumikia wakati wa uhai wake. Bwana ametoa! Bwana ametwaa Jina la Bwana lihimidiwe.

**Salamu za Pongezi**

**10.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** kama mtakumbuka, tarehe 16 Septemba 2024 Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alifanya uteuzi wa viongozi. Mheshimiwa Rais, alimteua Bw. Baraka Ildephonce Leonard kuwa Katibu wa Bunge na Bi Nenelwa Mwihambi kuwa Jaji wa Mahakama Kuu ya Tanzania.

**11.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** nami niungane na Mheshimiwa Spika pamoja na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kumpongeza sana Bwana Baraka Ildephonce Leonard kwa kuteuliwa kuwa Katibu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nimhakikishie kuwa Serikali itampa ushirikiano wote unaohitajika ili aweze kutekeleza majukumu yake.

**12.** ***Mheshimiwa Naibu Spika***, nitumie nafasi hii pia kumpongeza Mheshimiwa Jaji Nenelwa Mwihambi kwa uteuzi huo na nimtakie utekelezaji mwema wa majukumu yake mapya. Vilevile, ninamshukuru kwa kazi nzuri aliyoifanya wakati wote alipokuwa akilitumikia Bunge letu Tukufu.

**13.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** kipekee nampongeza sana Mheshimiwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani kwa kuongoza Mkutano wa 149 wa Umoja wa Mabunge Duniani uliofanyika kuanzia tarehe 13 Oktoba, 2024 huko Geneva, Uswisi. Mkutano huo, ulikuwa na lengo la kujadili kwa mapana kuhusu masuala yanayoathiri amani ya dunia, mazingira, haki za binadamu na demokrasia. Watanzania tuna kila sababu ya kijivunia ushupavu aliouonesha wakati wa Mkutano huo na jinsi alivyoonesha msimamo usioyumba wakati wote. Sina shaka uongozi wake utaweka alama katika historia ya uongozi wa Umoja wa Mabunge Duniani. Niwaombe Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wote kwa ujumla tuendelee kumuunga mkono Mheshimiwa Spika ili aendelee kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Sote kwa pamoja tumwombe Mwenyezi Mungu azidi kumpa uzima, hekima na nguvu katika kuutumikia Umoja wa Mabunge Duniani.

**SHUGHULI ZA BUNGE**

**14.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** Mkutano huu wa 17 wa Bunge la 12, ulipokea na kujadili taarifa mbalimbali kutoka kwa kamati za Kudumu za Bunge, maswali kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge na majibu ya Serikali sambamba na kujadili na kupitisha Mapendekezo ya Mpango wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 na Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**Maswali na Majibu**

**15.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** kupitia mkutano huu, Waheshimiwa Wabunge waliuliza maswali **133** ya msingi na mengine **491** ya nyongeza ambayo yalijibiwa na Serikali. Halikadhalika, maswali **Sita** ya papo kwa papo yaliulizwa na Waheshimiwa Wabunge na kujibiwa na Waziri Mkuu.

**Miswada ya Sheria**

**16.** ***Mheshimiwa Naibu Spika***, katika Bunge hili Serikali imewasilisha miswaada minne (04) ambayo ililetwa na kusomwa kwa mara ya kwanza. Miswada iliyowasilishwa ni kama ifuatayo:

**Moja**: Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 4 wa Mwaka 2024 (The Written Laws Miscellaneous Amendment of 2024).

**Mbili**: Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2024 (The Environmental Management (Amendment) Act, 2024).

**Tatu**: Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Kazi wa Mwaka 2024 (The Labour Laws (Amendments) Act, 2024) na

**Nne**: Muswada wa Sheria ya Uwekezaji na Maeneo Maalum ya Kiuchumi wa Mwaka 2024.

**Mapendekezo ya Mpango wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026**

**17.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** Serikali kupitia Ofisi ya Rais (Mipango na Uwekezaji) iliwasilisha Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2025/2026. Mpango huo umejikita katika kuendeleza na kukamilisha utekelezaji wa afua zinazotoa matokeo ya maeneo matano ya kipaumbele ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano.

**18.** **Mheshimiwa *Naibu* Spika,** vilevile, Mheshimiwa Waziri wa Fedha aliwasilisha Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026. Ikumbukwe kwamba, Mpango huo uliopitishwa na Bunge lako, ndiyo wa mwisho ambao unaenda kuhitimisha utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025.

19. **Mheshimiwa *Naibu* Spika,** nitumie fursa hii kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao katika Mpango huu pamoja na Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti kwa mwaka 2025/2026.

20. ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** Serikali kwa kushirikiana na Sekta Binafsi itaweka mkazo katika maeneo ya miradi ya kielelezo yenye manufaa na matokeo makubwa na kujielekeza katika vipaumbele vya mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2025/2026. Vipaumbele hivyo ni: kuchochea uchumi shindani na shirikishi; kuimarisha uwezo wa uzalishaji wa bidhaa viwandani na utoaji huduma; kukuza uwekezaji na biashara; kuchochea maendeleo ya watu; na kuendeleza rasilimaliwatu.

21. ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** niruhusu ninukuu maneno ya mwanatasnia ya filamu na muziki kutoka Marekani, Bi. Deborah K. Allen aliyesema (kwa tafsiri isiyo rasmi) "***Hata kama una bajeti kubwa kiasi gani, huwezi kufanya kila jambo***". Maana yake ni kwamba ni muhimu kuweka kipaumbele kwa masuala ya msingi ambayo yatakuwezesha kufikia ndoto zako, bila kujali kiasi cha fedha ulichonacho.

22. ***Mheshimiwa Naibu Spika***, ninatoa rai kwa watendaji wote Serikalini kuhakikisha vipaumbele vilivyoanishwa kwenye Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2025/2026 vinatafsiriwa vema kwenye mipango ya Taasisi zao ili kwa pamoja tuweze kufikia mwisho mwema wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025.

**Taarifa ya Kamati za PAC na LAAC kuhusu hesabu zilizokaguliwa na CAG kwa mwaka wa fedha 2022/2023 na Taarifa ya Kamati ya PIC kuhusu Uwekezaji na Mitaji ya Umma kwa mwaka wa fedha 2022/2023**

23. ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** Mkutano huu wa 17 wa Bunge lako umepokea na kujadili kwa kina Taarifa za Kamati za Bunge ikiwemo Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC), Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC), na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma (PIC) kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 ulioishia tarehe 30 Juni, 2023.

24. ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** taarifa hizi za Kamati zinazotokana na Taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Ninalipongeza Bunge lako tukufu kwa kuchambua kwa kina hoja zote za ukaguzi zinazohusu matumizi ya fedha za umma. Pamoja na kutoa maazimio ambayo kimsingi ni maelekezo mahsusi kwa Serikali.

25. ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** sote ni mashahidi kwamba, Serikali imeendelea kufanyia kazi mapendekezo yanayotolewa na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi chini ya uongozi wa Ndugu Charles E. Kichere, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Vilevile, Serikali imeendelea kuzingatia maelekezo yote yanayotolewa na Bunge lako tukufu kupitia maazimio na hoja zilizotolewa. Lengo la Serikali ni kuendelea kutoa huduma bora kwa wananchi kwa kuimarisha utamaduni wa uwajibikaji katika kusimamia na kudhibiti ipasavyo ukusanyaji wa mapato na matumizi.

26. ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** hoja zote zimeainishwa kwa ajili ya utekelezaji. Hivyo basi, ninaziagiza Wizara zote kuandaa kwa wakati taarifa za utekelezaji wa Maazimio yote kulingana na mapendekezo yaliyotolewa na Kamati za Bunge, na kuziwasilisha Ofisi ya Waziri Mkuu ili iweze kuwasilisha taarifa ya Serikali kwa Mheshimiwa Spika.

27. ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** napenda kuwakumbusha Maafisa Masuuli na Watendaji wote Serikalini kuhakikisha kuwa wanazingatia sheria, kanuni na taratibu za fedha za umma ili kutimiza ndoto na malengo ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya kuwaletea Watanzania maendeleo endelevu.

**MWENENDO WA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA KIPINDI CHA ROBO YA KWANZA YA MWAKA 2024/25**

28. ***Mheshimiwa Naibu Spika*, **Serikali imeendelea kusimamia makusanyo katika kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka 2024/2025 ambapo jumla ya **shilingi trilioni 11.55** zimekusanywa kutoka vyanzo vya ndani na nje ya nchi. Kati ya kiasi hicho, **shilingi trilioni 7.93** ni mapato ya ndani, sawa na **asilimia 99.4** ya lengo la kukusanya **shilingi trilioni 7.97**. Mapato hayo yanajumuisha mapato yaliyokusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania **shilingi trilioni 7.09**, mapato yasiyo ya kodi yaliyokusanywa na wizara na idara zinazojitegemea **shilingi bilioni 518.32**, na mapato kutoka vyanzo vya Mamlaka za Serikali za Mitaa **shilingi bilioni 321.32**.

29. ***Mheshimiwa Naibu Spika*,** mafanikio hayo yanatokana na mikakati mbalimbali iliyowekwa na Serikali. Mikakati hiyo ni pamoja na kuendelea kuimarisha na kuhimiza matumizi ya mifumo ya TEHAMA katika ukusanyaji wa mapato na kuhamasisha matumizi ya mashine za kutolea risiti za kielektroniki.

30. ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** nitumie fursa hii kuipongeza Mamlaka ya Mapato Tanzania inayoongozwa na Bw. Yusuph Mwenda na Taasisi zote zinazohusika katika ukusanyaji wa mapato kwa kazi nzuri wanayoifanya. Aidha, niwapongeze wananchi wote kwa kujitoa kwa dhati na kuhakikisha kuwa wanalipa kodi kwa ajili ya maendeleo ya taifa letu. Vilevile, wafanyabiashara wanapaswa kutoa risiti na wananchi kuhakikisha wanadai risiti kila wanaponunua bidhaa.

31. ***Mheshimiwa Naibu Spika*,** niwakumbushe watendaji wa Mamlaka ya Mapato Tanzania kuendelea kusimamia ukusanyaji wa mapato na utoaji wa elimu kwa wananchi kuhusu ulipaji wa kodi kwa manufaa ya nchi yetu. Kwa upande mwingine, nizikumbushe halmashauri zote nchini kuendelea kubuni vyanzo vipya vya mapato ili kuongeza wigo wa mapato ya ndani.

32. ***Mheshimiwa Naibu Spika*,** katika kipindi cha robo ya kwanza ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2024/2025, ridhaa ya **shilingi trilioni 11.67** ilitolewa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo. Matumizi ya kawaida yanajumuisha mishahara, kugharimia deni la Serikali na matumizi mengineyo.

33. ***Mheshimiwa Naibu Spika*,** matumizi ya maendeleo yamejumuisha kugharimia miradi na programu mbalimbali ikiwemo ujenzi wa reli ya kisasa (SGR); ujenzi na

ukarabati wa barabara, madaraja na viwanja vya ndege; Mradi wa Kufua Umeme wa Maji wa Julius Nyerere; miradi ya umwagiliaji; kuboresha Shirika la Ndege la Tanzania na mradi wa usambazaji umeme vijijini.

**34.** ***Mheshimiwa Naibu Spika***, matumizi mengine ni kuwezesha Mpango wa Elimumsingi Bila Ada; Mitihani ya darasa la saba pamoja na kidato cha nne; maandalizi ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa 2024; uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura na maandalizi ya mashindano ya kuwania Kombe la Mataifa ya Afrika.

**MASUALA YA UTABIRI WA HALI YA HEWA**

**35.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** mabadiliko ya tabianchi yamekuwa na athari ambazo tumekuwa tukizishuhudia. Msimu uliopita, nchi yetu iliathiriwa na vimbunga na mvua za EL-NINO. Kutokana na athari hizo, Serikali imechukua hatua muhimu za kurejesha hali kwa kukarabati miundombinu ya barabara, madaraja na makalavati yaliyoharibiwa.

**36.** ***Mheshimiwa Naibu Spika***, kipekee nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania kwa kuridhia matumizi ya fedha **shilingi bilioni 130** kwa ajili ya kurejesha miundombinu hiyo kwa dharura ambapo kazi zilifanyika usiku na mchana. Vilevile, kutumika fedha **shilingi bilioni 868.56** kwa ajili ya kujenga miundombinu ya kudumu ili kuhakikisha mawasiliano yanarejea.

**37.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** katika msimu huu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania ilitoa utabiri wa mwelekeo wa msimu wa mvua za vuli kwa kipindi cha kuanzia Oktoba hadi Desemba, 2024 na mwelekeo wa mvua za msimu zinazoanza Novemba, 2024 hadi Aprili, 2025. Kutokana na utabiri huo, msimu wa mvua za vuli unatarajiwa kutawaliwa na vipindi virefu vya ukavu na mtawanyiko wa mvua usioridhisha.

**38.** ***Mheshimiwa Naibu Spika***, tathmini inaonesha mvua za msimu zitakuwa za wastani hadi chini ya wastani na zinatarajiwa katika maeneo ya mikoa ya Kigoma, Tabora, Katavi, Rukwa, Songwe, Singida, Dodoma, Kaskazini na Mashariki mwa mkoa wa Lindi, na Kaskazini mwa mikoa ya Mbeya na Iringa.

**39.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** mvua za wastani hadi juu ya wastani zinatarajiwa katika mikoa ya Njombe, Ruvuma, Mtwara, maeneo ya Kusini na Magharibi mwa mkoa wa Lindi, Kusini mwa mikoa ya Mbeya, Iringa na Morogoro. Mvua nyingi zinatarajiwa katika kipindi cha nusu ya pili ya msimu ambacho ni Februari, 2025 hadi Aprili, 2025 ikilinganishwa na nusu ya kwanza ambacho ni Novemba, 2024 hadi Januari, 2025.

**40.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** kutokana na changamoto ya mabadiliko ya hali ya hewa na tabianchi, upo uwezekano wa kujitokeza vipindi vifupi vya mvua kubwa, mafuriko, upepo mkali, na ongezeko la joto. Hali hiyo inaweza ikasababisha athari mbalimbali ikiwemo uharibifu wa miundombinu. Nitumie fursa hii kuzielekeza Kamati za Maafa katika ngazi ya Kijiji, Wilaya, Mkoa na Taifa kujipanga kikamilifu kukabiliana na changamoto za mvua endapo zitajitokeza.

41. ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** nitoe rai kwa wakulima wote, kutumia mvua hizo kulima mazao yanayoendana na upatikanaji wa mvua katika maeneo yao na kuzingatia ushauri wa wataalamu wa kilimo. Kwa upande mwingine, Watanzania wote tuendelee kujenga tabia ya kufuatilia taarifa za utabiri wa hali ya hewa pamoja na kuzingatia maelekezo yanayotolewa na Serikali ikiwemo kuhama kwenye maeneo hatarishi na kufanya shughuli za kiuchumi na kijamii katika maeneo salama.

**Kuimarisha uratibu wa upatikanaji wa pembejeo**

42. ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** kwa kuwa tunaelekea katika msimu wa kilimo, ninaelekeza Mikoa na Halmashauri kuhamasisha wakulima kujisajili kwenye daftari la mkulima na kuwapatia namba za usajili. Pia, waendelee kuwahamasisha wauzaji wa pembejeo za kilimo kujisajili katika mfumo wa kidigitali ili waweze kuuza mbolea na mbegu bora za mahindi kwa wakulima kupitia utaratibu wa ruzuku.

***Mheshimiwa Naibu Spika***, kadhalika, niwaombe Waheshimiwa Wabunge wenzangu, mnaporejea kwenye majimbo yenu endeleeni kuwahimiza, wakulima wote wa zao la mahindi ambao hawajajisajili waende kujisajili kwenye daftari la mkulima. Daftari hilo linapatikana katika Ofisi za Vijiji/Mitaa. Wakulima watakaojisajili watapata namba maalum ya mkulima watakayoitumia kununulia mbolea na mbegu bora za mahindi.

**USIMAMIZI WA ELIMUMSINGI**

43. ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** ni dhamira ya Serikali kuhakikisha watoto wote wenye umri wa kuanza shule wanaandikishwa na kumaliza mzunguko wao wa masomo kwa mujibu wa ngazi husika. Lengo likiwa ni kuhakikisha tunajenga jamii ya Watanzania walioelimika, wenye maarifa, stadi na mtazamo chanya utakaowezesha kuchangia katika maendeleo ya Taifa letu.

44. ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** Serikali kwa sasa inaendelea na maandalizi ya uandikishaji wa wanafunzi wa Elimu ya Awali na Darasa la Kwanza kwa kutumia maoteo yanayotokana na takwimu za Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022. Matarajio ni kuandikisha watoto wa Elimu ya Awali zaidi ya **milioni 1.8** na wanafunzi wa darasa la Kwanza wapatao **milioni 1.7**.

45. ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** zoezi la uandikishaji limekwishaanza, nitoe wito kwa wazazi na walezi kuhakikisha wanawaandikisha watoto wote wenye umri wa kuanza shule wakiwemo watoto wenye mahitaji maalum.

46. ***Mheshimiwa Naibu Spika***, naelekeza Wakurugenzi wa Halmshauri zote kuwapangia majukumu Watendaji wa Vijiji na Kata wawahamasishe wazazi na walezi pamoja na viongozi katika makundi ya kijamii ili wanafunzi wote waliofikia umri wawe wameandikishwa.

47. ***Mheshimiwa Naibu Spika***, vilevile, tunaratajia kupokea wanafunzi watakaoanza Kidato cha Kwanza kuanzia Januari, 2025. Ili kuhakikisha wanafunzi

hao wanaanza masomo kwa wakati mmoja, ninaelekeza Viongozi wa Mikoa na Wakurungezi wa Halmashauri zote kusimamia kikamilifu ujenzi wa miundombinu kwa ajili ya kuwapokea wanafunzi hao ifikapo Januari, 2025.

## HALI YA UTOAJI WA MIKOPO YA ELIMU YA JUU

**48.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** Serikali katika kuhakikisha upatikanaji wa fursa za masomo ya elimu ya juu pamoja na taaluma za kipaumbele kwenye vyuo vya kati, imeendelea kutenga fedha kwa ajili ya kutoa mikopo ya wanafunzi. Katika mwaka wa fedha 2024/2025, imetenga jumla ya shilingi **bilioni 787.4** kwa ajili ya wanafunzi **245,799** ambapo hadi sasa jumla ya shilingi **bilioni 600.6** zimetolewa kwa wanafunzi **189,641.**

**49.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** pamoja na Serikali kuendelea kuongeza fedha za kukopesha wanafunzi, kumekuwa na ongezeko la wahitaji wa mikopo hiyo. Ili kukabiliana na changamoto hii, Serikali inaangalia uwezekano wa kuishirikisha sekta binafsi katika ugharimiaji wa elimu ya kati na ya juu.

## MAANDALIZI YA UCHAGUZI WA VIONGOZI WA SERIKALI ZA MITAA

**50.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** uandikishaji na maandalizi ya orodha ya wapigakura wa Uchaguzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa ni takwa la Kanuni za Uchaguzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa za mwaka 2024. Kanuni hizo zinaelekeza kuwa, kutakuwa na orodha ya wapigakura ambayo itatumika katika uchaguzi wa mwenyekiti wa kijiji, mwenyekiti wa mtaa, mwenyekiti wa kitongoji na wajumbe wa serikali za vijiji na kamati za mitaa.

**51.** ***Mheshimiwa Naibu Spika*****,** nitumie fursa hii kuwapongeza wananchi kwa kujitokeza kwa wingi wakati wa uandikishaji. Vilevile, nitoe rai kwa wananchi wote kama walivyojitokeza kwenye kujiandikisha vivyo hivyo wajitokeze siku ya Jumatano, tarehe 27 Novemba, 2024 kupiga kura.

## MAELEKEZO MAHSUSI

### Nishati Safi ya Kupikia

**52.** ***Mheshimiwa Naibu Spika*****,** kama mnavyofahamu kuwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amekuwa mstari wa mbele katika kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia. Katika Mkutano wa 79 wa Baraza la Umoja wa Mataifa uliofanyika Septemba, 2024, Mheshimiwa Rais alipongezwa kwa kuwa kinara katika kuhakikisha malengo ya kuhamia kwenda nishati safi ya kupikia yanatimia ifikapo mwaka 2030.

**53.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** kwa umahiri wa Mheshimiwa Rais, Tanzania imeombwa na kukubali kuwa mwenyeji wa Mkutano wa Ngazi ya Juu wa Nishati Afrika utakaofanyika tarehe 27 hadi 28 Januari, 2025. Lengo la mkutano huo ni kuhamasisha ushirikiano mpana wa kufikisha nishati ya umeme kwa watu milioni 300 barani Afrika ifikapo mwaka 2030.

**54.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** jana (Novemba 6, 2024) niliamua kutembelea taasisi zetu hapa Dodoma zikiwemo Kambi ya JKT Makutupora, Shule ya Sekondari ya Wasichana Msalato na Gereza la Isanga kwa ajili ya kufuatilia utekelezaji wa maelekezo ya Mheshimiwa Rais kuhusu matumizi ya nishati safi na salama. Mambo niliyoyabaini ni haya yafuatayo:

(i) Kambi ya JKT Makutupora na makambi yote ya JKT yametekeleza maelekezo ya Mheshimiwa Rais kwa kujenga mifumo ya gesi (LPG) kwa ushirikiano wa Kampuni ya Taifa Gas. Pia kwa kushirikiana na Wakala wa Nishati Vijijini (REA) wanatekeleza mradi utakaowapatia majiko banifu na sufuria zake 291 kwa vikosi vyote, majiko ya gesi na sufuria zake 180, mitambo ya biogas tisa na majiko yake, mashine za kutengeneza mkaa mbadala 60 ambapo mafunzo kwa vijana kuhusu mitambo hii yataendeshwa na REA.

(ii) Shule ya Sekondari ya Wasichana Msalato imetekeleza maelekezo hayo kwa kujenga mifumo inayotumia mkaa mbadala ujulikanao kama KUNIPOA ambao unatengenezwa kwa kutumia maganda ya miwa na takataka za miti ambao umewasaidia kupunguza sana gharama za uendeshaji kuliko ilivyokuwa awali. Nilielezwa kwamba zamani walikuwa wakitumia shilingi milioni 4.5 kila mwezi ili kununua kuni za kawaida, lakini kwa sasa wanaokoa shilingi milioni 1.3 kwa kutumia KUNIPOA.

(iii) Gereza Kuu la Isanga chini ya Jeshi la Magereza limeanza kutumia majiko banifu kwa kutumia mkaa RAFIKI unaotengenezwa na STAMICO. Jeshi hilo linaendelea kutekeleza mpango wa matumizi ya nishati safi ya kupikia chakula cha wafungwa na mahabusu magerezani ambao utahusisha vituo 211 yakiwemo magereza 129, Ofisi 26 za Magereza za Mikoa na Vyuo vya Magereza vinne, Makao Makuu, Bohari Kuu, Hospitali kuu ya Jeshi, Karakana, Shule ya Sekondari Bwawani, Kikosi Maalum na Kambi za Magereza 47.

**55.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** Serikali inaendelea kuweka msisitizo wa matumizi ya nishati safi ya kupikia kwa msingi huo nielekeze masuala yafuatayo:

(i) Taasisi zote zenye kuandaa chakula cha watu zaidi ya 100 zihakikishe zinatekeleza maagizo haya ya kuhamia kwenye matumizi ya nishati safi ya kupikia;

(ii) Wizara ya Nishati iendelee kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa Mkakati wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia;

(iii) Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya kote nchini, wafanye ukaguzi kwenye taasisi zilizomo katika maeneo yao mathalan majeshi, polisi, vyuo vya elimu ya kati na ya juu, vyuo vya wizara mbalimbali kama elimu, afya na kilimo kwani ni maeneo yanayopaswa kubadilisha mifumo yao ya nishati ya kupikia kwa vile yana idadi kubwa ya walaji wa vyakula. Aidha, wajasiriamali wanaopika chakula cha watu wengi kama vile kwenye harusi wahamasishwe ili nao wabadilishe teknolojia zao ili ziendane na matumizi ya nishati safi ya kupikia.

(iv) Ninawaelekeza Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya wote ifikapo Desemba, mwaka huu watoe taarifa ya utekelezaji kuonesha ni taasisi ngapi tayari zimetekeleza agizo hilo, hii ni kwa taasisi zote za umma na binafsi. Lengo ni kuhakikisha kuwa ifikapo mwaka 2033 asilimia 80 ya Watanzania wawe wanatumia nishati safi ya kupikia ambayo ni: Gesi, umeme, vumbi la makaa ya mawe, Kunipoa zinazotokana na takataka.

(v) Wananchi waendelee kubadili mfumo wa maisha hususan taratibu za kupika chakula ili kuachana na nishati chafu ya kupikia inayohusisha kuni na mkaa unaotokana na miti.

**MICHEZO**

**56.** ***Mheshimiwa Naibu Spika***, Serikali ya awamu ya sita imeendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ya kuhakikisha kuwa sekta ya sanaa, utamaduni na michezo imeendelea kuleta tija na mafanikio makubwa hapa nchini.

**57.** ***Mheshimiwa Naibu Spika***, mikakati inayofanywa na Serikali imekuwa chachu ya mafanikio tunayoendelea kuyashuhudia katika sekta ya michezo. Mikakati hiyo ni pamoja na kuendelea kutenga fedha katika bajeti ya kila mwaka ili kufanikisha mipango ya maendeleo ya sekta hiyo.

**58.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** bajeti ya Sekta ya michezo imeongezeka kufika **shilingi bilioni 285.31** katika mwaka 2024/2025 ikilinganishwa na **shilingi bilioni 54.74** katika mwaka wa fedha 2021/2022. Ongezeko hilo ni kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya viwanja na huduma saidizi kwa ajili ya maandalizi ya mashindano ya AFCON 2027.

**MAANDALIZI YA AFCON 2027**

**59.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** kama mtakumbuka Waheshimiwa Wabunge, Serikali imeshaanza mchakato wa maandalizi ya mashindano ya AFCON yanayotarajia kufanyika mwaka 2027. Hatua za maandalizi zinatekelezwa kwa kuzingatia mpango mkakati wa utekelezaji wa maandalizi ya mashindano ya AFCON 2027. Miongoni mwa masuala yanayotekelezwa katika mpango Mkakati huo ni pamoja na: ujenzi na ukarabati wa miundombinu; uendelezaji wa masoko ya utalii; uandaaji wa timu ya taifa; ulinzi na usalama pamoja na mpango wa matangazo na hamasa kwa umma.

**60.** ***Mheshimiwa Naibu Spika***, kwa upande wa miundombinu, Serikali inatekeleza miradi ya ujenzi wa viwanja vya michezo ikiwemo kiwanja cha Arusha. Vilevile, inakarabati viwanja vya Benjamin Mkapa, Uhuru na Amani - Zanzibar ili kukidhi vigezo vya mashindano ya CHAN yanayotarajiwa kufanyika Februari, 2025 na AFCON 2027. Aidha, Serikali inaendelea na ukarabati wa viwanja mbalimbali vya mazoezi vitakavyotumika katika mashindano hayo.

**PONGEZI KWA WASHINDI WA MICHEZO MBALIMBALI**

**61.** ***Mheshimiwa Naibu Spika***, nitumie fursa hii kutoa pongezi zangu za dhati kwa wanamichezo wote walioshiriki katika mashindano mbalimbali kitaifa na kimataifa na kulileta Taifa letu heshima kubwa. Kama ***wahenga walivyosema***

***asiyekubali kushindwa si mshindani***, nitoe rai kwa wanamichezo ambao hawakufanikiwa kupata ushindi wajipange upya kwa ajili ya kushiriki katika mashindano mengine.

**62.** ***Mheshimiwa Naibu Spika***, nianze kutoa pongezi zangu kwa mshindi wa mchezo wa ngumi, mwanamasumbwi Abdul Ramadhan Ubaya ambaye katika pambano la *light heavy weight* lililofanyika tarehe 25 Oktoba, 2024 nchini Urusi alifanikiwa kumshinda kwa *knock out* bondia Ibragim Estemirov kutoka Urusi. Vilevile, nitumie fursa hii kuwapongeza mabondia wengine ambao wamekuwa wakifanya vizuri katika mashindano mbalimbali.

**63.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** kipekee ninaipongeza Timu ya Taifa ya Wanaume ya Mchezo wa Kriketi kwa kufuzu mzunguko wa pili wa Mashindano ya Wanaume ya ICC Ukanda wa Jangwa la Sahara yatakayofanyika Machi, 2025. Ninawapongeza sana kwa ushindi huo na kuwatakia kila la heri katika hatua inayofuata.

**64.** ***Mheshimiwa Naibu Spika***, tumeendelea kushuhudia wachezaji wa mpira wa miguu wakifanya vizuri katika mashindano mbalimbali ndani na nje ya nchi. Nianze kwa kuwapongeza Timu ya Taifa ya Vijana chini ya miaka 12 kwa kufanikiwa kutinga katika nusu fainali ya mashindano ya *Female Universal Youth Cup* yaliyofanyika Dingnan, nchini China.

**65.** ***Mheshimiwa Naibu Spika,*** ninaipongeza pia, Timu ya Taifa ya Wavulana chini ya miaka 16 kwa kushika nafasi ya pili katika mashindano ya FIBA Kanda ya tano Afrika yaliyofanyika hivi karibuni. Wakati huo huo, Timu ya Taifa ya Vijana chini ya miaka 20 (*Ngorongoro Heroes*) imetwaa kombe la CECAFA baada ya kuishinda timu ya Rwanda mabao 3 kwa 1. Vilevile, katika mashindano ya nusu fainali yaliyofanyika tarehe 18 Oktoba, 2024 uwanja wa KMC jijini Dar es Salaam na kufuzu AFCON 2025 baada ya kuifunga Timu ya Kenya chini ya miaka 20 mabao 2 kwa1.

## USHIRIKI WA VILABU VYETU KWENYE MASHINDANO YA KIMATAIFA

**66.** ***Mheshimiwa Naibu Spika***, vilabu vya Tanzania vimeendelea kufanya vizuri katika mashindano ya kimataifa, ambapo kwa msimu wa mwaka 2023/2024 Tanzania ilifanikiwa kuingiza timu nne. Katika mashindano ya Klabu Bingwa Afrika timu mbili za Azam na Yanga na katika Kombe la Shirikisho timu mbili za Simba na Coastal Union. Aidha, Timu za Yanga na Simba zimefanikiwa kuingia hatua ya makundi katika mashindano ya Klabu Bingwa na Shirikisho. **Ninazipongeza na tunawatakia mafanikio mema kwa ligi ya NBC, vilabu vinaendelea vizuri kupambana.**

## SHUKURANI NA KUTOA HOJA

**67.** ***Mheshimiwa*** **Naibu Spika,** ninapoelekea kuhitimisha hotuba yangu, nitumie fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Spika, na zaidi ya yote kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa kuchangia mjadala wa Bunge hili kwa kuzingatia manufaa makubwa ya ustawi wa Taifa letu. Kama mnavyofahamu uwepo wa Bunge hili ulikuwa ni muhimu ili kuweza kupata maoni na ushauri

kutokana na hoja za Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na Mapendekezo ya Mpango wa Taifa wa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**68.** ***Mheshimiwa*** **Naibu Spika,** vilevile, ninamshukuru Katibu wa Bunge, wasaidizi wake na watumishi wote wa Bunge kwa huduma nzuri walizotupatia kwa kipindi chote tulichokuwa tukitekeleza majukumu yetu ya Mkutano wa 17 wa Bunge la 12. Pia, ninawashukuru viongozi na watendaji wa Serikali na taasisi zake kwa kuendelea kufanyia kazi masuala mbalimbali ambayo yamekuwa yakiwezesha uwasilishaji wa hoja zilizotokana na mijadala ya Bunge. Ninavishukuru pia vyombo vya ulinzi na usalama kwa kuendelea kuhakikisha mikutano ya Bunge inaendelea kufanyika katika hali ya utulivu na amani.

**69.** **Mheshimiwa Naibu Spika,** kipekee, ninawashukuru wanahabari kwa kufanya uchambuzi mzuri wa hoja na mwenendo mzima wa Bunge na pia kwa kuwahabarisha wananchi. Kadhalika, ninawashukuru madereva waliotuhudumia wakati wote tukiwa hapa Bungeni.

**70.** ***Mheshimiwa Naibu Spika*****,** kwa kuwa tunaelekea mwishoni mwa mwaka, na hatutakuwa na mkutano mwingine ndani ya mwaka 2024, nitumie nafasi hii kuwatakia Waheshimiwa Wabunge, Watanzania na waumini wote wa Kikristo, sherehe njema ya sikukuu ya Krismasi na heri ya mwaka mpya wa 2025. Niwatakie safari njema Waheshimiwa Wabunge wote mnaporejea majimboni kwenu na Mwenyezi Mungu awafikishe salama kwenye vituo vyenu vya kazi.

**71.** ***Mheshimiwa Naibu Spika*****,** baada ya maelezo hayo, ninaomba kutoa hoja kwamba Bunge lako tukufu liahirishwe hadi tarehe **28 Januari, 2025** siku ya Jumanne, saa tatu kamili asubuhi katika ukumbi huu hapa jijini Dodoma.

**72.** ***Mheshimiwa Naibu Spika*****,** sasa, ninaomba kutoa hoja.